BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kuendelea kukutana katika Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nitoe shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa miongozo na kuelekeza vyema muelekeo wa sekta ya elimu Zanzibar inayosisitiza watoto wetu wapate elimu bora itayowawezesha kujitegemea. Pia, Natoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Riziki Pembe Juma, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mmanga Mjengo Mjawiri kwa mashirikiano makubwa wanayoendelea kuipatia Kamati hii na kuyathamini maoni ya Kamati kwa kuyazingatia vyema. Nachukua nafasi hii kuwaomba waendelee kutupa mashirikiano kwa lengo la kuiimarisha zaidi sekta hii muhimu ya elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Ustawi wa Jamii inatoa pongezi za dhati kabisa kwa kauli mbiu ya mwaka huu inayosema "ELIMU BORA KWANZA" , tunaomba kauli mbiu hii ifanyiwe kazi kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa michango yao mikubwa wanayoendelea kuipatia Wizara na hasa katika

kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba niwatambue wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dr Mwinyihaji Makame Mwadini | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Tatu Mohammed Ussi | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hidaya Ali Makame | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Makame Said Juma | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Massoud Abrahman Massoud | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Aziza Wazir Kheir | Katibu |
| 9. | Ndg. Khamis Hamad Haji | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyojua kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo chanzo kikuu cha kuzalisha wataalamu wa fani mbali mbali ambao Serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali zinawatumia katika shughuli mbali mbali za maendeleo ya nchi yetu ambayo upatikananji wake ni kwa kuongeza bidii na nyenzo madhubuti za kiuchumi pamoja na kuwaendeleza wataalamu wetu katika kada mbali mbali za utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuanzisha Kamati maalum ya madawati. Jambo hili ni la muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya skuli nyingi za hapa nchini zinakabiliwa na upungufu wa madawati kwa muda mrefu. Aidha tunatoa pongezi za dhati kabisa, kutokana na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na suala hilo ambapo matunda ya juhudi hizo kwa sasa yanaonekana kutokana na muitikio uliooneshwa na taasisi mbali mbali za kiserikali na zisizo za kiserikali. Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua fursa hii adhimu kuwasomba zaidi washirika mbali mbali wa maendeleo na wananchi wote kwa ujumla kuzidisha juhudi kwa kuchangia zaidi ili tatizo hili liweze kuondoka katika skuli zetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilitoa rai kuwa fedha zinazochangishwa kwa ajili ya ununuzi wa madawati zisiekwe benki tu bali zianze kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, kwa vile lengo tumeshalijua basi madawati yaanze kutengenezwa japo kidogo kidogo, kuepuka kuongezeka kwa gharama za utengenezaji. Madawati hayo

baada ya matengenezo yahifadhiwe sehemu hadi yatakapotimia yapelekwe katika skuli husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu imeridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha sekta ya elimu hapa nchini kutokana na miradi mbali mbali ya kimaendeleo iliyokwishakamilika na ile ambayo bado ujenzi wake unaendelea. Hata hivyo, Kamati inatoa tahadhari kwa kuiomba Serikali kuwa makini na utendaji wa Wakandarasi ambao baadhi yao hutoa maelezo yanayoridhisha na kuziwezesha kampuni zao za ujenzi kushinda tenda lakini wanapokabidhiwa maeneo ya kazi hushindwa kukamilisha kazi kwa wakati kutokana na udhaifu wao wa kutumia fedha wanazolipwa na SMZ kuzitumia kwenye miradi yao mengine. Pia Kamati inaiomba Serikali ijitahidi kutoa fedha kwa wakati katika miradi ambayo inafadhiliwa na Serikali ili miradi hiyo ikamilike kwa muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** tunafahamu kuwa nchi yetu ni masikini na inachukua juhudi mbali mbali katika ukusanyaji wa mapato ili ihakikishe kuwa bajeti tunayoipanga kwa ajili ya matumizi yetu inatusaidia kwa kiasi kikubwa. Pamoja na juhudi hizo zinazochukuliwa na Serikali, Kamati yangu inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuhakikisha kuwa hiyo bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara zetu na ambayo imeidhinishwa na Baraza lako tukufu, ipatikane kwa wakati kama ilivyoidhinishwa. Pia Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kujipanga katika kudhibiti na kubuni zaidi vianzio vipya vya mapato ili bajeti yetu isiwe tegemezi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu imeamua kuyaeleza haya kutokana na kilio kikubwa kilichopo katika Wizara tunazozisimamia, naamini hata Wizara nyengine ambapo hali ya kukosekana kwa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa katika bajeti kwa wakati, fedha ambazo zimeshaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ni kilio cha muda mrefu katika Wizara hizo na Kamati yangu imeona ni vyema kulibainisha hili ili Serikali ilijue na ilifanyie kazi.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo inajidhihirisha katika bajeti iliyopita ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, jumla ya shilingi 69,407,825,847 za SMZ zilipatikana kwa kazi za kawaida na maendeleo ambazo ni sawa na 50%. Hii inadhihirisha wazi kuwa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa katika bajeti si mzuri sana, hivyo tunaiomba Serikali izidishe juhudi katika upatikanaji wa fedha hizo.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufikia malengo yake ya kunyanyua viwango vya elimu kwa wanafunzi wetu, inapaswa kuweka mipango madhubuti itakayosaidia kufanikisha kupatikana kwa malengo yaliyokusudiwa kwa lengo la kutoa huduma bora katika sekta ya elimu na hatimaye kupelekea upatikanaji wa elimu iliyo bora. Suala la uwiano mzuri wa mwalim kwa mwanafunzi hasa katika elimu ya maandalizi na msingi, tunashauri liangaliwe kwa undani

**Mheshimiwa Spika**, kazi kubwa ya Wizara ni kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata taaluma ya kutosha itakayoisaidia Serikali kufikia malengo yake ya kuondokana na changamoto ya ukosefu wa elimu iliyo bora, changamoto ambayo Wizara inapaswa kuzidisha juhudi za makusudi kwa kuwazidishia ujuzi walimu wa skuli ili kuipunguza na hatimaye kuiondoa kabisa kadhia hii katika taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inalizungumzia suala la upatikanaji wa elimu bora kwa kuzingatia hali halisi tuliyoikuta katika baadhi ya skuli ambazo tulizitembelea wakati wa ziara za Kamati. Kamati yetu katika ziara zake ilitembelea skuli mbali mbali ikiwemo na Skuli ya Kinuni ambapo hali ya skuli hiyo hairidhishi kutokana na mazingira magumu yaliyopo kwa walimu na wanafunzi. Kamati ilisikitishwa sana na ufinyu wa nafasi skulini hapo ambapo kwa mwaka 2016/2017 wanafunzi wa darasa la kwanza pekee walioandikishwa hawapungui wanafunzi 800. Hali hiyo imepelekea kuwa na watoto wa darasa la kwanza wapatao 294. Hali hii inadhihirisha ugumu uliopo wa mazingira ya kufundishia na kupokea elimu inayotolewa,hivyo Wizara na Serikali kwa ujumla pamoja na juhudi zake inapaswa kuweka mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu ya matatizo hayo ambayo yanaonekana ni changamoto kubwa na yatakapoondoka matatizo hayo basi kwa kiasi kikubwa wanafunzi wetu watajengewa misingi mizuri ya kupata elimu iliyo bora.

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2017/2018 ambao unaendelea kutumia utaratibu wa kibajeti ulioanza kutumika mwaka juzi ambao umeelekea katika utekelezaji wa program (Programme Based Budget, PBB). Mfumo huu umepengwa kuwezesha Wizara hii kusimamia program sita ambazo ni kama ifuatavyo:

(1.) Elimu ya Maandalizi na Msingi;

(2.) Elimu ya Sekondari;

(3.) Elimu ya Juu;

(4.) Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;

(5.) Ubora wa Elimu; na

(6.) Programu ya Utawala na Uongozi.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo huu wa kibajeti ni mzuri endapo utasimamiwa vizuri na taasisi husika, utawezesha baadhi ya changamoto zilizopo katika taasisi hizo kutatuka kwa haraka na endapo upatikanaji wa fedha zilizotengwa zitapatikana kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri na kuiomba Serikali ijitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kuwa inakamilisha malengo yote ya Wizara yaliyopangwa. Hata hivyo, Kamati inazidi kusisitiza na kuitaka Wizara kuwabana wakandarasi wote wanaopewa kazi na Serikali kwa lengo la kuzikamilisha kazi hizo kwa wakati ili kuondoa usumbufu pamoja na kuondoa hasara ambayo inaweza kutokea kutokana na ucheleweshwaji wa kazi.

## ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa pongeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi zake kubwa za kuwalea watoto wetu vizuri na kuwapatia chakula wanafunzi wa skuli za maandalizi pamoja na kuondoa kabisa malipo na michango yote katika ngazi ya elimu ya msingi. Kamati inatoa pongezi kutokana na utekelezaji wa jambo hili ambalo linawasaidia watoto kusoma kwa utulivu pamoja na kuwaondolea wazazi na walezi mzigo wa malipo na michango ambayo kwa namna moja ama nyengine ilikua inawapa shida sana wananchi walio wengi wa kipato cha chini ambao wengi wao walikua hawamudu gharama hizo. Kamati inaiomba Wizara kufuatilia kwa makini baadhi ya skuli ambazo bado zinaendelea kuwachangisha wanafunzi wa skuli za msingi kinyume na maagizo na maelekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaiomba Wizara kuimarisha zaidi huduma za msingi katika skuli za maandalizi ili wazazi na walezi wahamasike kuwapeleka watoto wao katika skuli hizo wanapofikisha umri wa kwenda skuli. Kamati inachukua nafas hii pia kuwasisitiza wazazi kuwapeleka watoto wanapofikia umri wa kwenda skuli za maandalizi ili kwenda samabamba na sera ya elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri sana Wizara kukaa pamoja na Kamati za Wazee maskulini kusikiliza changamoto zao  na kutafuta namna ya kuzitatua changamoto hizo ambazo baadhi yake zipo mikononi mwa wazee kama utoro na upungufu au mmong’onyoko wa maadili kwa vijana wetu.

## ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ina majukumu makubwa yakiwemo ya kusimamia upatikanaji mzuri wa elimu kwa watoto wetu pamoja na kuhakikisha kuwa kupitia Bodi yake ya Mikopo ya Elimu ya juu inawapatia mikopo wanafunzi wote wenye sifa na vigezo vya kupatiwa mikopo hiyo. Kamati yangu inapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na timu yake yote kutokana na juhudi walizozichukua za kuwataka wale wote waliokopeshwa waanze kulipa mikopo wanayodaiwa na bodi ili wanafunzi wengine waweze kunufaika na mkopo unaotolewa na Serikali.

**Mheshmiwa Spika,** Juhudi hizo za Mheshimiwa Waziri zimepelekea urudishwaji wa mikopo hiyo kuwa katika hali ya kuridhisha na hadi hivi sasa jumla ya wanafunzi 108 wamemaliza kabisa madeni yao, aidha hadi kufikia mwezi April mwaka huu jumla ya wanafunzi wanaoendelea kurejesha mikopo yao ni wanafunzi 1387, idadi hii inaridhisha sana kutokana na hali ilivyokua huko mwanzoni. Kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia mwezi April jumla ya Tshs Milioni 845 zilirejeshwa ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/2017 jumla ya wanafunzi 594 walipatiwa mikopo kwa ajili ya kuendelea na masomo yao idadi ambayo ikijumlishwa na wale wanaoendelea, ambao ni wanafunzi 2072 idadi ambayo inapelekea kuwa na jumla ya wanafunzi 2666, jumla ya Tshs Bilioni 6.1 zimetumika kugharamia mikopo hiyo. Katika kikao cha Kamati na Wizara, Kamati ilielezwa kuwa wanafunzi wanaopokea mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka uliopita walikuwa ni asilimia 20 na kwa mwaka huu Wizara imepanga kutoa mikopo kwa asilimia 40 ya wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na wanafunzi wengi waliowahi kupatiwa mikopo kuanza kuitikia wito wa Serikali na kuanza kulipa madeni yao, Kamati inasisitiza zoezi hili la kuwatafuta wadaiwa wa mikopo liwe ni endelevu kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliopewa mikopo kutolipa madeni yao pamoja na kwamba wameshamaliza kusoma. Kamati imeelezwa kuwa jumla ya wanafunzi 4958 wanadaiwa japokuwa baadhi yao katika hao wameanza kulipa.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni kuwasaidia wanafunzi ambao hawana uwezo wa kujilipia. Hivyo ni haki ya kila Mzanzibari mwenye sifa na vigezo kupatiwa mkopo na kunufaika na mkopo huo kwa kujiongezea taaluma. Kamati imebaini kuwa tokea kuanzishwa kwa Bodi, jumla ya wanafunzi 7624 tayari wamenufaika na fursa ya mikopo kutoka Bodi ya Mikopo, idadi ambayo si kubwa sana ukilinganisha na mahitaji yaliyopo. Kutokana na hali hiyo, Kamati

inashauri Wizara kuendelea na juhudi zake za kusimamia kikamilifu zoezi la kuwasaka wale wote waliokopeshwa na ambao hawajalipa ili waweze kurejesha mikopo waliyopewa na Serikali ili na wanafunzi wengine waweze kunufaika.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na baadhi ya wanafunzi waliopatiwa fursa hii kutolipa madeni yao, Kamati yangu imefarijika sana na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika bajeti ya mwaka huu ya kuongeza fedha kidogo katika bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu jambo ambalo litasaidia wanafunzi wengi zaidi kupatiwa mikopo na Serikali kwa lengo la kuendelea na masomo yao. Mwaka huu zimetengwa jumla ya Tshs Bilioni 10.1 ukilinganisha na mwaka jana ambapo zilikua ni bilioni 6.1. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi mikopo hazitoshi, hivyo, bajeti ya mwakani pia izingatie uongezwaji wa fedha katka Bodi ya Mikopo.

**Mheshimiwa Spika,** ilivyokuwa wanafunzi walio wengi walioomba kupatiwa mkopo na Bodi ni wanyonge, hivyo si vyema kwa Bodi kuwacheleweshea kuwaingizia fedha unapofika wakati unaotakiwa. Kucheleweshwa kuingizwa fedha za matumizi na mambo mengine ya msingi unapelekea usumbufu mkubwa kwa wanafunzi wenyewe hasa wanafunzi wa kike wanaosoma nje ya Zanzibar. Hivyo, Bodi inapaswa kuwa makini kwa kuhakikisha kuwa inawapatia wanafunzi mikopo yao kwa wakati unaostahiki, Wizara haina budi kujipanga vizuri kuomba pesa mapema kutoka Wizara ya Fedha..

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo Kamati yetu inapenda kuchukua nafasi hii kufikisha salam za pongezi kutoka katika Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki kiliopo Dar es salaam, kutokana na mashirikiano yaliyopo baina ya Wizara na chuo hicho katika suala zima la ulipaji wa mikopo ya wanafunzi. Pamoja na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo lakini uongozi wa chuo hicho, ulitoa taarifa kwa Kamati kuwa pale malipo ya wanafunzi yanapochelewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huchukua juhudi ya kuandika barua kwa ajili ya kuujuulisha uongozi wa chuo kuwa malipo ya wanafunzi yatachelewa lakini hatimaye deni hulipwa.

## UKAGUZI MASKULINI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Ustawi wa Jamii imebaini kuwa ukaguzi katika skuli za Serikali na binafsi unafanyika na Kamati imeridhishwa na maelezo iliyopatiwa na Wizara wakati wa kupitia bajeti ya Wizara hii. Hata hivyo, Kamati yangu inaiomba Wizara kufanya ukaguzi wa mara mara kutokana na baadhi ya walimu kutotekeleza wajibu wao ipasavyo, Kamati inapendekeza ukaguzi kwa skuli za Serikali ufanyike kwa kuwapeleka wakaguzi watakaotoka maeneo tofauti na eneo lililokusudiwa kukaguliwa. Jambo hili litapelekea ufanisi mkubwa katika kazi za ukaguzi maskulini kwa vile matarajio yetu kwa

kuwepo wakaguzi wa mbali kutapunguza mwanya wa kuoneana haya wa kuficha ukweli wa uhalisia wa mambo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na juhudi hizo tunaiomba Wizara iwanunulie nyenzo za kufanyia kazi wakaguzi wote ili kuwaondolea usumbufu unaojitokeza kwa baadhi ya wakaguzi kukosa vitendea kazi ikiwemo usafiri.

## MAKTABA NA MAABARA KATIKA SKULI

**Mheshimiwa Spika,** Maktaba ni eneo muhimu katika skuli zetu ambapo wanafunzi wanatarajiwa kuitumia vizuri fursa hiyo na kujiongezea taaluma na ujuzi wa kile walichofundishwa darasani na walimu wao. Kamati yangu inachukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Wizara na Serikali kutokaa na uamuzi wake wa kuweka kipaumbele cha kuzijengea Maktaba na Maabara skuli 23 za Unguja na Pemba. Uamuzi huu ni wa maana sana hasa ikizingatiwa kuwa wanafunzi wanahitaji kuongeza ujuzi na maarifa ya kile walichofundishwa darasani pamoja na kufanya majaribio ya yale waliyofundishwa ili kuongeza uwezo na ufahamu wao.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maamuzi hayo, Kamati yangu inapenda kutoa angalizo kwa Wizara kujipanga katika upatikanaji wa fedha za ununuzi wa vifaa vya maabara kutokana na changamoto kubwa inayozikabili skuli nyingi hapa nchini za ukosefu wa vitendea kazi. Wazo la kuzijengea skuli maabara ni zuri na ni wazo la msingi sana katika kuwaendeleza wanafunzi wetu katika masomo ya sayansi, hata hivyo, tunazidi kusisitiza kuwa fedha kwa ajili ya kununulia vitendea kazi vya maabara hizo ni muhimu kupatikana kama ilivyopangwa ili maabara hizo zifanye kazi kama ilivyokusudiwa.

## HUDUMA ZA MAJI KATIKA SKULI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekua ikifanya jitihada mbali mbali kwa kujenga skuli mpya na kuzikarabati baadhi ya skuli ambazo zika katika hali mbaya. Pamoja na jitihada hizo suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni muhimu na linapaswa kupewa kipaumbele cha hali ya juu kutokana na mahitaji ya huduma hiyo kwa wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika**, mvua za mwaka jana zilisababisha athari kubwa miongoni mwetu na kupelekea kuzuka kwa maradhi ya mripuko ya kipindupindu. Kutokana na umuhimu wa suala la upatikanaji wa maji katika kujikinga na maradhi haya, Kamati yangu inazidi kusisitiza umuhimu wa Wizara kuweka visima katika skuli zote za zamani na mpya

zinazojengwa hivi sasa . Kamati inasisitiza suala hilo kutokana na uhalisia uliotokea mwaka jana ambapo maradhi ya mripuko yalipelekea skuli nyingi kufungwa kuepusha kuenea kwa maradhi ya kipindupindu. Hivyo, ni vyema suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama likapewa kipaumbele kujikinga na athari zinazoweza kutokea.

## BAJETI YA WIZARA NA UAJIRI WA WALIMU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuajiri wafanyakazi 260 ambao kwa kiasi Fulani watasaidia kuziba pengo kubwa la walimu lililokuwepo katika skuli zetu. Pamoja na juhudi hizo, Kamati bado inasisitiza kuwa suala la uajiri liwe endelevu kila nafasi zinapopatikana kutokana na mzigo mkubwa walionao baadhi ya walimu kwa sababu ya ukosefu wa walimu hasa wa masomo ya sayansi na hisabati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea taarifa kuwa suala la upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti limekua na changamoto kubwa, kukosekana kupatikana kwa wakati fedha zote zilizoidhinishwa kunaathiri kwa kiwango kikubwa utendaji wa Wizara. Hivyo, Kamati inashauri sana Serikali ifanye juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa zinapatikana kwa wakati kuiendeleza sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaiomba Serikali kuliangalia kwa undani suala hili ili nguvu na juhudi tunazozichukua za kuwaletea wananchi wetu maendeleo ziweze kufanikiwa na hatimaye watoto wetu waweze kupata elimu iliyo bora. Vituo vya Mafunzo ya Amali ni miongoni mwa taasisi muhimu ambazo zinahitaji fedha za kutosha kwa ajili ya kuviendeleza vituo hivyo hasa suala la upatikanaji wa vitendea kazi na uboreshaji wa vyumba vya kazi (workshop) pamoja na kutoa ujuzi na elimu iliyo bora kwa vijana wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu, Vituo vya Mafunzo ya Amali vilikua havipati fedha za maendeleo (SDL) kwa ajili ya kuviendeleza, jambo ambalo lilikua ni kilio cha muda mrefu. Katika kila ziara za Kamati, jambo hili lilikua likilalamikiwa na wahusika na Wizara ilikua ikipewa taarifa ya kufuatilia fedha hizo ambazo zimekua zikitengwa kwa ajili ya kuviendeleza vituo vya amali lakini zilikua hazipatikani. Hata hivyo, kutokana na juhudi zilizochukuliwa na Wizara, katika bajeti ya mwaka huu, Kamati imeelezwa kuwa fedha hizo zitapatikana kwa ajili ya kuviendeleza vituo hivyo, jumla ya Tshs 10,846,047,000 zimetengwa kwa mwaka 2017/2018. Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na watendaji kutokana

na juhudi walizochukua. Hata hivyo, Kamati inaiomba Wizara kusimamia upatikanaji wa fedha hizo na tunaiomba Serikali izitoe fedha hizo kwa wakati. Aidha Kamati inaishauri Serikali katika bajeti inayokuja kuhakikisha fedha za SDL zinapatikana kwa kasma ile ile iliyowekwa na sheria ya Mamlaka ya vyuo vya Amali.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2017/2018 katika Baraza lako tukufu. Pia nawashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao kila panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoibua wakati wa mjadala.

**Mheshmiwa Spika,** Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha. Ahsanteni.

…………………………………….

**Mwanaasha Khamis Juma,**

**Kny: Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar.</u>**